
Globethics Repository

# Mkataba wa Watu wa Dunia
# [Charter of the Peoples of the Earth]

This page was generated automatically upon download from the Globethics Repository. More information on Globethics see https://www.globethics.net. Data and content policy of Globethics Repository see https://repository.globethics.net/pages/policy.

| | |
|---|---|
| Item Type | Preprint |
| Authors | "Forum for a New World Governance (FnWG) Citizens Regional Assemblies" |
| Rights | With permission of the license/copyright holder |
| Download date | 2026-06-17 00:53:51 |
| Link to Item | http://hdl.handle.net/20.500.12424/213555 |

# Mkataba wa Watu wa Dunia
## Rasimu ya kwanza



*Januari 2011*
*Kama unataka kuchangia katika mjadala*
*na kuboresha pendekezo hilo,*
*unaweza kujisajili kwa kuandika kwa:*
*carta@forums.rio20.net*

**Mkataba wa mradi wa kuunganisha watu pamoja na kuanza mjadala**

Katika nyakati hizi za mashaka na changamoto ya kimataifa, ni muhimu kwamba wanainchi, wanaume na wanawake ambao hufanya watu tofautitofauti wa Dunia waweza kuunda hatua yao na kuendeleza kwa pamoja kanuni ambazo zinaongoza jitihada za binadamu katika karne ya ishirini na moja.

Je, ni lazima watu kutoka Afrika, Marekani, Asia, Uropa na Oceania kusubiri kwa ajili ya wengine kuamua, bila ridhaa yao au kwa niaba yao, juu ya misingi ya kimaadili ambayo itakuwa ikijengwa katika sura ijayo ya jitihada za dunia? Je, wao wenyewe wanaweza ridhika na ushindi, ndani ya mipaka yao na wakati mwingine kwa msaada wa taasisi za kimataifa,vitisho ambazo wanajamii huleta duniani wao wenyewe kama vile usugu wa umaskini uliokithiri, ukolezi wa mali na nguvu, na vikwazo vingine kwa ujumla ambazo zimerithiwa kwa njia ya historia ya muda mrefu wa vita na migogoro?

Safari ya kufungua njia ya binadamu aliyekombolewa imeanza. Kuna ufahamu kuhusu ugeuzi mkubwa ambao unakabili ulimwengu. Kwa muda mrefu, watu wamegawanyika, ingawa kwa umoja na mara kwa mara wamefurahia pamoja ushirika wao, ujasiri, hekima na ubunifu ili kuweza kupitia vikwazo vya historia pamoja. Katika ukweli wa mambo,wao tayari ni wajumbe na viongozi halisi wa maadili mapya, utamaduni, siasa na jamii ambazo zimejengwa kwa muda huu wote kutokana na makosa, ubunifu, mivutano na migogoro waliyopitia. Sasa wao na watendaji wahusika wana haki ya kujadili maswala muhimu ambayo inawaleta pamoja, ili waweze kuongea kwa maneno yao na kuwaza jinsi ya kuishi katika jamii kwa heshima na kwa amani na Mama Dunia.

Mkataba ufuatao ndio mpango wa kwanza na mwaliko wa kuzungumza. Inaweza kuimarishwa, kurekebishwa, na kubadirishwa kulingana na mahitaji na mazungumzo yanayofanyika katika mfumo wa maandalizi ya Mkutano wa Dunia wa 2012 na baadaye. Nakala inaangazia juu ya Mkataba wa Uhuru (Freedom Charter) wa kihistoria, ambao ulizaliwa Mjini wa Afrika Kusini, na kwamba umekuwa bendera kwa ajili ya harakati za kupambana na ubaguzi wa rangi (anti-apartheid) na uliopitishwa mwaka wa 1955 na Shirikisho la Watu (Congress of the People). Mkataba uliandikwa na timu ya uratibu ya Jukwaa la Utawala mpya wa Dunia (Forum for a new World Governance) na Mikoa ya Bunge za Raia (Citizens Regional Assemblies), kwa kushiriki na kuhusika katika harakati za watu zinazoendelea katika bara mbalimbali.

*"Kuwa huru sio tu kutupa minyororo yako,*
*lakini ni kuishi kwa njia inayoheshimu*
*na kuboresha uhuru wa watu wengine"*
*Nelson Mandela*



## Wakati vitisho kubwa zina uzito juu ya dunia yetu na sisi wenyewe,

Wakati  mabilioni ya watu wanadhulumiwa kila siku kwa njia zinazodhoofisha madhara ya umaskini uliokithiri,
Wakati nchi yetu pamoja na serikali hawana uwezo wala upendo wowote wa kukubaliana kutekeleza ufumbuzi unaofaa na kwa wakati ufaao kwa hatari zinazotisha dunia yetu na sisi wenyewe,
Wakati Umoja wa Mataifa na mashirika yanayotokana nalo au wameshikamana nalo daima hawana fedha, nyenzo na njia za kisiasa za kukabiliana na vitisho hivi kwa ufanisi au kuzitokomeza,
Wakati Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki kuu ya Dunia (World Bank) pamoja na makampuni ya kimataifa ambayo hayajakosa uwezo wa kutatua matatizo tu, lakini ndio wanaosababisha matatizo haya.

## Sisi watu wa Afrika, Marekani, Asia, Uropa na Oceania, sayari yetu yote na wanaume na wanawake ambao wanaishi juu yake tunatangaza,

Ya kwamba nchi yetu ni Mama Dunia na kwamba Ulimwengu ni nchi yetu,
Ya kwamba umaskini wa baadhi ni umaskini kwa wote,
Ya kwamba aibu ya baadhi ya udhalilishaji kwa wote,
Ya kwamba hofu ya baadhi ni hofu kwa wote,
Ya kwamba utumwa wa baadhi ni utumwa kwa wote.

## Ya kwamba pamoja, tunatengeneza ushirika wa watu tofautitofauti

Ambao ni huru na wanawajibika, na kusimama katika mshikamano,
Ambao katika tofauti zao zilizokithiri, na katika umbali wao mkubwa,
Hawagawanyiki katika nyakati za tofauti zinazozotokana na kulishwa na chuki iliyochochewa kihistoria,

Na vikwazo bandia vya mara nyingi vya mipaka ya taifa, na kwa kukosekana kwa haki na usawa ambao unagomea baadhi ya nchi badala ya wengine,
Baadhi ya mikoa badala ya mingine, baadhi ya jamii badala ya nyingine, baadhi ya watu binafsi badala ya wengine,
Ambao bado wanaamini kwamba maisha yao ya karibu na mbali hutegemea kushinda vikwazo hivi vyote vilivyotokana na historia ya muda mrefu wa vita na migogoro ambayo itakuwa na mwisho wakati sura ingine ya jitihada kubwa ya binadamu itakapoanza,
Kama moja ya kusisimua na kuahidi ambayo inatisha kwa changamoto na uhakika inayotoa.

## Sisi tunathibitisha kwamba tutafanya kazi na tutapigana daima kuona:

Kila binadamu atakuwa na haki sawa bila ubaguzi wa umbali, rangi, jinsia, utamaduni, kabila au taifa,
Kila binadamu afaidike kutoka mwanzo kwa fursa sawa,
Kila binadamu awe na uhuru wa kushiriki katika dini yake na kushikilia imani yake hata wale ambao hawana dini,
Kila binadamu atakuwa na uhuru wa kutoa maoni yao mahali popote pale katika sayari,

## Kila binadamu aweze kupata utajiri na rasilimali ya dunia yetu,

Bila kujali mahala walikozaliwa au makaazi, au mahali mali na rasilimali zinatoka,
Kila binadamu awe na uwezo wa kupata mfumo wa elimu unaostahili pamoja na watoto wao wote,
Kila binadamu awe na uwezo wa kupata huduma za afya kwa haraka na ambazo zinakubaliana na hali yake ya afya,
Kwa Kila binadamu aweze kupata maji na lishe anayohitaji kwa ajili ya kuishi, afya yao na kwa ustawi,

## Kila binadamu aweze kuandaa na kushiriki katika maisha ya kisiasa ya kijiji, nchi, mkoa au dunia yao,

Kila binadamu lazima apate mfumo wa kisheria wananchi wote wa dunia kwa usawa, bila kujali asili yao,
Kila binadamu awe na haki ya kuhamia mahali popote duniani bila kuzingatia taifa analotoka,
Kila binadamu aweze kupata ajira kulingana na sifa yake, mahali popote duniani, bila kujali mahala walikozaliwa.

## Kila binadamu awe na uwezo wa kuishi katika hadhi na heshima,

Katika usalama na faraja, kwa furaha na kulingana na dhana yao ya furaha,
Kwa binadamu wote, nishati na rasilimali za fedha hatimaye kuchangia katika kupigana na umaskini ili pamoja kwa utulivu tuweze kujenga maisha yetu ya baadaye.
Mwisho, ni wajibu wetu sote katika moyo wa ushirika na uwajibikaji, kufanya haki hizi kupatikana na kuheshimiwa bila mgawanyiko wowote.

## Kuondolewa kwa mmoja wetu na binadamu wote kushutumiwa.

Watu wakiunganishwa pamoja lazima waongoze dunia!
Kwa hivyo tutapigana pamoja, upande kwa upande, mpaka mwisho wa vikwazo, mpaka ukombozi wetu utakapopatikana na tuweze kuishi kwa amani na Mama Dunia, katika hadhi na uhuru.

Watu wa dunia, kwa muda mrefu tumegawanyika.
Wakati umefika wa kufungua fursa ya binadamu huru.